



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO
BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA



25 Februari, 2025

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA CHA MCHEZO WA KUOGELEA KWA WATU
WENYE ULEMAVU (TPSA).

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwataarifu wanachama na wadau wa Chama cha Kuogelea kwa Watu wenye Ulemavu (TPSA) kuwa, uchaguzi wa viongozi wa chama hicho unatarajiwa kufanyika tarehe 06 aprilii, 2025, Jijini Dar es salaam.

Fomu za kugombea nafasi tofauti katika uchaguzi huo zitaanza kutolewa katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Benjamin Mkapa na zinapatikana katika tovuti ya Baraza ambayo ni www.bmt.go.tz kuanzia Jumatano tarehe 26 Febr - 02 Aprili, 2025.

Aidha, Usaili wa wagombea wa nafasi tofauti unatarajiwa kufanyika Ijumaa ya tarehe 04 Aprili, 2025 katika Ofisi za Baraza kabla ya uchaguzi huo eneo hilohilo.

Nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na:

Nafasi	Ada
1. Mwenyekiti	
2. Makamu wa Mwenyekiti	
3. Katibu Mkuu	
4. Mweka Hazina	
5. Mkurugenzi wa Ufundi	
6. Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo	
7. Wajumbe watatu (3) wa kamati ya utendaji	50,000/=

Sifa za wagombea

- i. Awe Raia wa Tanzania
- ii. Awe na elimu isiyopungua Kidato cha nne (cheti cha Elimu ya Sekondari)
- iii. Awe na ujuzi na uzoefu wa uendeshaji wa michezo wa kuogelea uliothibitishwa wa angalau miaka miwili (2).
- iv. Asiwe na hatia yoyote ya kosa la jinal na kuhukumiwa kifungo jela bila uchaguzi wa faini.
- v. Awe na umri usiopungua miaka ishirini na tano (25)
- vi. Awe amewahl kuwa ama mchezaji wa kuogelea, Kocha, Mwamuzi, Klongozi au kushiriki katika uendeshaji wa michezo wa kuogelea.

- vii. Awe amehudhuria mafunzo mbalimbali ya uongozi na menejimenti ya michezo yanayotambuliwa nchini.
- viii. Mtu anayegombea nafasi ya Mwenyekiti/Makamu wa TPSA lazima awe na uzoefu mzuri na uliothibitishwa wa angalau miaka mitano (5) katika uendeshaji wa michezo wa kuogelea na awe na uwezo, uadilifu, haiba ya hadhi ya kuwakilisha TPSA ndani nan je ya Tanzania.
- ix. Mgombea ye yeyote lazima awe anaishi nchini Tanzania.

Malipo ya fomu yafanyike katika akaunti ya Baraza, kwa kutumia mfumo mpya wa malipo ya Serikalini.

Ili kupata namba malipo mgombea anashauriwa kupiga namba ya simu ifuatayo; 0713 380 499

Aidha, fomu ya kugombea iwasilishwe Baraza ikiambatishwa na risiti ya malipo pamoja na nakala za nyaraka kulingana na sifa mahususi zilizoainishwa katika katiba ya TPSA.

BMT inatoa wito kwa yeyote mwenye sifa kwa mujibu wa katiba ya chama cha michezo wa kuogelea kwa watu wenye ulemavu kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi huo na maendeleo ya Mchezo huu nchini.

Imetolewa Na:



Najaha Bakari

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano.